

## On-site Education of Practical Languages for Area Studies

### Report in 2008

—Swahili & Maasai, University of Nairobi, Kenya, 20 Nov. 2008 - 20 Apr. 2009—

Year of Enrollment: 2008

Graduate School of Asian and African Area Studies

Sakiko Sone

#### On My Swahili Language Training (Swahili)

##### I. Maisha ya shule yangu

Nilijifunza Kiswahili kwa muda wa miezi miwili, kwanzia mwezi wa kumi na mbili 2008, mpaka mwezi wa kwanza 2009, katika shule ya lugha ya kanisa la kiangilikana la Kenya, Nairobi. Shule hii inatoa mafunzo ya lugha tofauti katika Kenya, kwa mfano Kimaasai, Kiluo, Kiturkana na kadhalika. Wanafunzi hao wanatoka nchi mbalimbali kama vile Ulaya, Afrika, Asia, Marekani na Arabuni.

Mimi, nilikuwa mwanafunzi wa darasa la kwanza. Nilisoma Kiswahili pamoja na wanafunzi wenzangu wawili kutoka Uitaliano na Rwanda ambaye wanafanya kazi ya hiari huko vibandani. Mwalimu wetu alitufundisha habari za sarufi ya msingi, matamko na insha. Baada ya masomo kutoka saa kumi (4pm), nilitembea mjini, Nairobi, na marafiki zangu kutoka Kenya kila siku. Kwa wakati wa likizo, niliwatembelea nyumbani kwao na nikapata nafasi ya kujulikana na kuongea na watu wengi kwa Kiswahili.

Nairobi ina maeneo kama themanini. Kila eneo ina tofauti yake. Wakati wa kukaa Nairobi, nilitembelea maeneo kama ishirini na tano pamoja na marafiki wangu. Moyo yangu ilipendezwa kabisa kwa maeneo za nguvu, kama vile Ngara, Kamukunji, Pumwani na Starehe. Fundi wa kienyeji wengi wanatengeneza vyombo mbalimbali wakati wote hapo. Mahali hapo pana soko nyingi na wenyeji wengi sana. Shabaha langu ni kutembelea maeneo yote katika Nairobi, na kujionea sehemu mbalimbali za Nairobi.

##### II. Kiswahili

Kiswahili ni lugha ambayo inazungumzwa na watu kutoka Afrika Mashariki, kama vile Kenya, Tanzania, Uganda na baadhi ya sehemu za Zaire, Rwanda, Burundi na kadhalika. Kiswahili ni “Lingua Franca” kwa kupelekana



⟨ ↑ shule yangu, kanisa la kiangilikana ⟩



⟨ ↑ mwalimu, wanafunzi wenzangu na mimi ⟩

habari mahali popote watu wanapoongea lugha mbalimbali. Unaweza kusikiliza Kiswahili sanifu kabisa katika sehemu za pwani na visiwa kama Zanzibar na Mombasa. Lakini Nairobi na barani zingine mbali na pwani, watu wengi wanaongea Kiswahili kwa jinsi tofauti na watu wa pwani. Kwa mfano, watu wa Nairobi hushangaa sana Kiswahili chako sanifu kama vile, “Samahani” ”Bila shaka” na ”Naomba,” ambazo ni kawaida pwani. Aidha watu wa Nairobi wanachanganya Kiwahili na Kiingereza pamoja mara nyingi. Zaidi ya hayo, wanaongea sheng.



〈 ↑ rafiki zangu wanakunywa pombe, Kayole, nairobi〉

Sheng ni lugha mpya ambayo imeanzishwa mjini, Nairobi, na inachanganywa na lugha zingi zinazosemwa hapo kama Kiswahili, Kiingereza, lugha za kabila kama vile Gikuyu na Kiluo, na lugha za Ulaya zingine. Sheng inatumiwa kwa kawaida na vijana, lakini imeenezwa mpaka vizazi vingine, kwa sababu wanaweza kusikia sheng popote katika Nairobi, kama vile kwa basi, muziki za umma, redio na program za runinga. Nataka kusoma sheng zaidi mara ingine ili nipate upelekeaji laini wa habari na watu wa mtaa. Ingawa watu wengi wa Nairobi wanaweza kusema Kiingereza vizuri, wanatumia Kiswahili na sheng kwa mazungumzo ya kila siku, kwa sababu ni lugha ya kupendeza.